**TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MAJUKUMU YA RUWASA KATIKA HALMASHAURI YA WILAYA YA ARUSHA KATIKA KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBA, 2022**

**1.0 Utangulizi**

Katika kipindi cha robo ya Kwanza (Julai – Septemba) ya mwaka wa fedha 2022/2023 shughuli za sekta ya maji ziliendelea kama kawaida katika maeneo ya kazi za kawaida za RUWASA na zile za miradi ya maendeleo kwa muhtasari taarifa hii inaeleza kazi zilizofanyika katika kipindi cha robo ya Kwanza ya mwaka wa fedha 2022/2023 na hali halisi ilivyo katika maeneo yafuatayo:-

- Utekelezaji wa miradi ya maji inayotumia fedha za mfuko wa maji (NWF)
- Utekelezaji wa miradi ya maji inayotumia fedha za malipo kwa matokeo awamu ya 5 (PbR V)
- Utekelezaji wa miradi ya maji inayotumia fedha za Uviko - 19

**1.1 Utekelezaji wa miradi ya maji inayotumia fedha za mfuko wa maji (NWF)**

Kwa kipindi cha Julai - Septemba RUWASA imeendelea kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa miradi ya ujenzi wa miundombinu ya maji katika mradi wa maji Olmulo na mradi wa maji losikito. Aidha kwa mradi wa uboreshaji wa Olmulo Mkandarasi ameshakabidhiwa eneo la kazi (site) na sasa anafanya kujiridhisha sehemu ambazo bomba la maji litapita kabla ya kuanza kuchimba "re survey".

*- Kwa maelezo ya kina kwa Miradi inayoendelea kwa fedha za mfuko (NWF) tazama kiambatanishoNa.1*

**1.2 Utekelezaji wa miradi ya maji inayotumia fedha za malipo kwa matokeo awamu ya 5 (PbR V)**

Katika kipindi cha Julai - Septemba Ruwasa Arumeru tuliendelea na utekelezaji wa miradi ya ukarabati na upanuzi katika vijiji vya Manyire, marurani, majimoto pamoja na mradi wa maji wa old Nduruma.

*-Kwa maelezo ya kina kwa miradi ya malipo kwa matokeo awamu ya tano (PbR V) Tazama kiambatanisho Na.2*

**1.3 Utekelezaji wa mradi unaotumia fedha za uviko - 19**

Kwa kipindi cha mwezi Julai - Septemba ofisi ya Ruwasa wilaya ya Arumeru iliendelea na utekelezaji wa mradi unaojengwa kwa fedha za uviko – 19 ambao ni upanuzi wa mradi wa maji Likamba kwenda lesiraa na Olchorovous.

*-Kwa maelezo ya kina kwa miradi inayotekelezwa kwa fedha za uviko-19 tazama kiambatanishoNa 3.*

**Naomba kuwasilisha.**

Inj. Shabir I. Wazir
**KAIMU MENEJA WA RUWASA**
**WILAYA YA ARUMERU**



Generated by CamScanner

TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO KWA FEDHA ZA PbR V KWA KIPINDI CHA JULAI HADI SEPTEMBA 2022- RUWASA ARUMERU. Kiambatanisho No.2

| Na | Jina la Mradi | Thamani ya Mradi | Tarehe ya kuanza mradi | Tarehe ya kumaliza mradi | Fedha zilizopokelewa | Fedha zilizotumika | Kazi zilizopangwa kufanyika | Kazi zilizofanyika Kwa kipindi cha Julai - Septemba 2022 | Changamoto | Utatuzi wa changamoto | Asilimia ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Mradi wa maji Manyire marurani na majimoto | 250,000,000.00 | 09/01/2021 | 30/07/2022 | 200,000,000.00 | 207,077,000.00 | Uchimbaji na ulazaji wa bomba umbali wa mita 5,000. | Uchimbaji na ulazaji wa bomba umbali wa mita 4500, kazi inaendelea | Hakuna | Hakuna | 90 |
| 2 | Mradi wa maji Old Nduruma | 176,095,911.00 | 07/01/2022 | 30/12/2022 | 176,095,911.00 | 147,524,000.00 | Uchimbaji wa mtaro na ulazaji wa bomba umbali wa mita 2,000 | Uchimbaji wa mtaro na ulazaji wa bomba umbali wa mita 1,975 imeshafanyika. | Uvushaji wa bomba kwenye barabara ya east africa | Tuko kwenye mchakato wa kumpata mzabuni atakayetoboa barabara ili kuvusha bomba | 90 |
| | JUMLA | 426,095,911.00 | | | 376,095,911.00 | 354,601,000.00 | | | | | |

Generated by CamScanner

AARIFA YA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAJI INAYOFADHILIWA KWA FEDHA ZA MFUKO (NWF) KWA KIPINDI CHA JULY HADI SEPTEMBA 2022 - RUWASA ARUMERU. Kiambatisho Na. 1

| a la Mradi | Thamani ya Mradi | Tarehe ya kuanza mradi | Tarehe ya kumaliza mradi | Fedha zilizopokelewa | Fedha zilizotumika | Kazi zilizopangwa kufanyika | Kazi zilizofanyika Kwa kipindi cha Julai Hadi Septemba 2022. | Asilimia ya utekelezaji |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| adi wa maji OLMULO | 4,611,002,211.95 | 20/09/2022 | 20/03/2023 | - | - | Ujenzi wa chanzo cha maji, ujenzi wa vilula 2 vya maji, uchimbaji na ulazaji wa bomba umbali wa mita 46,000. | mkandarasi ameshakabidhiwa eneo la kazi (site) na sasa anafanya kujiridhisha sehemu ambazo bomba la maji litapita kabla ya kuanza mradi. | 0 |
| adi wa maji Losikito | 2,599,248,383.64 | 30/12/2020 | 30/06/2023 | 850,000,000.00 | 801,185,507.75 | Ujenzi wa nyumba 2 za kuendeshea pampu (pamp house),ununuzi na ufungaji wa pampu 3 za kusukuma maji aina ya submersible, ujenzi wa tank moja la kuhifadhia maji lenye mita za ujazo 225, ujenzi wa matank 2 ya kupokelea maji (sump tank) yenye mita za ujazo 100 kwa kila moja, ujenzi wa bomba kuu lenye urefu wa mita 10,000. kujenga mabomba ya usambazaji yenye umbali wa mita 23,151. Ujenzi wa vilula 24 vya kuchotea maji, ujenzi wa birika 2 za kunyweshea mifugo. | Ujenzi wa nyumba ya pili ya kuendeshea pampu (pump house No. 2), ujenzi wa tank namba 2 la kupokelea maji (sump tank na. 2), na ujenzi wa uzio | 35 |
| JUMLA | 7,210,250,595.59 | | | 850,000,000.00 | 801,185,507.75 | | | |

Generated by CamScanner